

TANGAZO LA SERIKALI Na. 226 la tarehe 11/7/2014

**SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA**

(SURA YA 290)

---

**SHERIA NDOGO**

---

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

---

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA  
BUSOKELO, ZA MWAKA 2014

**SEHEMU YA I  
UTANGULIZI**

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo za Mwaka, 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokua pale itakapoelezo vinginevyo; - “Ada na Ushuru” maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

“Afisa Muidhiniwa” maana yake ni Afisa yejote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

“Chombo cha Usafiri” maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa mkokoteni, au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo.

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya

Busokelo.

- “Kibali” maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.
- “Kituo cha Mabasi” maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremsha abiria na mizigo ya Abiria.
- “Machinjio” maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi.
- “Maegesho” Sehemu ye yote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda utakaotajwa na Halmashauri au tiketi za kuegeshea.
- “Masoko” maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa.
- “Mnada” maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza na kununua bidhaa.
- “Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo pamoja na Afisa ye yote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.
- “Usajili wa vyombo vy ya usafiri” maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vy ya usafiri vinyofanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmashauri.
- “Ushuru wa Madini ya Ujenzi” maana yake ni ushuru utakaotozwa kwa kibali cha uchimbaji wa Kokoto, Mawe, Changarawe, Mchanga, Chokaa, Marumalu, Kifusi, Udongo Mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi;
- “Wakala” maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni, au asasi ye yote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

#### SEHEMU YA II NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Ada na –  
Ushuru

- 4.-(1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru mbalimbali kwa ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na Ushuru atatozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya huduma kutolewa.

(3) Huduma zitakazotozwa Ada na ushuru katika Sheria Ndogo hizi ni:-

- (a) Ada ya kukodisha mali za Halmashauri;
- (b) Ada ya machinjio, ukaguzi wa nyama na ushuru wa Bucha;
- (c) Ushuru wa Mazao mchanganyiko;
- (d) Ushuru wa stendi na maegesho;
- (e) Ushuru wa Samaki;
- (f) Ada ya kuendesha shughuli za utamaduni, burudani na michezo;
- (g) Ada ya matangazo ya biashara;
- (h) Ada ya upimaji wa ardhi na vibali vya ujenzi;
- (i) Ada na Ushuru kwa huduma nyingine.

(4) Halmashauri itatenga maeneo maalumu ya kutoza Ada na Ushuru kutohana na chanzo husika.

(5) Malipo ya Ada na Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Wajibu wa  
kulipa Ada na  
Ushuru

5.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru kuhakikisha kwamba analipa Ada na Ushuru kwa viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni.

(3) Malipo ya Ada na Ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri au Wakala na mlipa Ada na ushuru.

***Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi***  
***Tangazo la Serikali Na. 226 (linaendelea)***

---

Uteuzi wa  
wakala

6.-(1) Halmashauri ina Mamlaka ya kumteua mtu binafsi, kampuni, Asasi au Taasisi kukusanya Ada na Ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeulewa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:-

- (a) kukusanya na kupokea Ada na Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;
- (b) kuwasilisha makusanyo yote aliowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala;
- (c) Wakala aliyeulewa kukusanya mapato ya Halmashauri atatakiwa kuweka dhamana ya kusanyo la mwezi mmoja kabla ya kusaini Mkataba.
- (d) Kusanyo la mwezi mmoja lililowekwa dhamana na wakala litarejeshwa mwisho wa mwaka wa fedha unahusika na Mkataba.
- (e) Kuilipa Halmashauri kiwango cha uwakala kilichokubaliwa katika mkataba siku tano (5) kabla ya tarehe ya kuanza uwakala Kwa kila mwezi;
- (f) kumchukulia hatua za kisheria mtu ye yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi;

**SEHEMU YA III**  
**MAKOSA NA ADHABU**

Makosa  
na  
Adhabu

7. Itakuwa ni kosa kwa:-

(1) Kwa Wakala;

(a) kukusanya Ada na Ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba toka kwa Halmashauri;

- (b) kujaribu au kukusanya ada na ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa na Sheria Ndogo hizi;
- (c) kushindwa kuwasilisha au kuwasilisha pungufu ya kiwango cha Ada na Ushuru alichokubaliwa katika mkataba; atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi elfu hamsini au Kifungo kwa kipindi cha miezi kumi na miwili jela au vyote viwili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) Kwa yejote;

- (a) Akishindwa, akidharau, au akikaidi/ Atakataa kulipa Ada na Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa Ada na Ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi;
- (b) Akimshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada na Ushuru;
- (c) Akitengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji, au ataturza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada na Ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri;
- (d) Kwa makusudi huku akijua ni kosa atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, au Atashindwa au kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;
- (e) akishindwa kuweka Kumbukumbu, Vitabu, Hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika Halmashauri; na
- (f) Akimzuia Afisa Muidhiwa au Wakala kutekeleza majukumu yake.

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi hamsini elfu (50,000/=) au kutumikia kifungo kisichozidi Miezi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

***Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi***  
***Tangazo la Serikali Na. 226 (linaendelea)***

Kufifilisha kosa      8. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yejote faini isiyozidi shilingi laki moja (100,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa faini iliyoainishwa chini ya Jedwali la Nane la Sheria Ndogo hizi.

**YAMEUNDWA CHINI YA KIFUNGU CHA 4 (1)**  
**JEDWALI LA KWANZA**

**I. ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI**

<i>Na.</i>	<i>Huduma</i>	<i>Kiwango</i>
1.	Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya mikutano/ vikao na sherehe	200,000/= kwa siku
2.	Kukodi viti	400/= kwa siku
3.	Kukodi Gari: Magari makubwa bila mafuta	200,000/= kwa siku
4.	Mitambo (Trekta, Total station, Vifaa vyatya GPS na kadhalika)	500,000/= kwa siku
5.	Vibanda vyatya biashara ; Soko la Kandete, Iwangwa, Ntaba na Mbambo	30,000/= kwa mwezi
	Mzunguko wa Lwangwa Stendi na Kandate Maeneo mengine	30,000/= kwa mwezi 20,000/= kwa mwezi

**II. ADA NA USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO**

<i>Na.</i>	<i>Zao</i>	<i>Kiwango</i>
1.	Viazi	1,000/- kwa gunia la debe sita
2.	Kabichi	500/= kwa gunia la debe sita au 7,500/=kwa tani moja
3.	Ndizi	200/= kwa kila mkungu au 10,000/= kwa tani moja
4.	Mahindi	300/= kwa kila debe moja au 3,000/= kwa gunia la debe kumi.
5.	Mpunga	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko kwa kila debe moja
6.	Mchele	300/= kwa kila debe moja

***Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi***  
***Tangazo la Serikali Na. 226 (linaendelea)***

7.	Maharage	300/= kwa kila debe moja
8.	Njegere	300/= kwa kila debe moja
9.	Maembe/Machungwa/Machenzena na parachichi	2,000/= kwa gunia la debe sita
10.	Tangawizi	6,500/= kwa gunia la debe sita
11.	Karoti	1,000/= kwa gunia la debe sita
12.	Ufuta na Iriki	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko kwa kilo moja
13.	Ngano	2,000/= kwa gunia la debe sita
14.	Vitunguu swaumu	5,000/= kwa gunia la debe sita
15.	Vitunguu maji	3,000/= kwa gunia la debe sita
16.	Nyanya	500/= kwa tenga moja dogo
17.	Nyanya	1000/= kwa tenga moja kubwa
18.	Alizeti/Mtama/Ulezi	2000/= kwa gunia la debe sita
19.	Mazao mengine yasiyotajwa	1000/= kwa gunia la debe sita
20.	Magimbi/mihogo	1000/= kwa gunia la debe sita
21.	Nyungo	200/= kwa kila ungo

**III. ADA YA HUDUMA ZA MACHINJIO, UKAGUZI WA NYAMA NA USHURU WA BUCHA**

<i>Na.</i>	<i>Ada/Ushuru</i>	<i>Kiwango</i>
1.	Ada ya Machinjio na Ulaguzi wa nyama kwa kila Ng'ombe atakayechinjwa	Kwa bei ya kilo moja
2.	Ada ya Machinjio na Ulaguzi wa nyama kwa kila Kondoo, Mbazi na Nguruwe atakayechinjwa	Kwa bei ya kilo moja
3.	Kuuza,kuchoma nyama mnadani	1,500/= kwa siku
4.	Ushuru wa bucha la N'gombe, Mbazi, Kondoo, Nguruwe na Samaki	1000/= kwa siku

**IV. ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTAMADUNI, BURUDANI NA MICHEZO**

<i>Na.</i>	<i>Ada/Ushuru</i>	<i>Kiwango</i>
1.	Kibali cha vikundi vyta ngoma za kibiashara	30,000/= Kwa kibali
2.	Kibali cha kuchezesha disco, Maonyesho ya bendi, Sanaa za maonyesho	30,000/= Kwa onyesho

***Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi***  
***Tangazo la Serikali Na. 226 (linaendelea)***

3.	Kibali cha kuchezesha Michezo ya Kubahatisha	30,000/= Kwa kibali
4.	Kibali cha kuchezesha filamu/kuigiza	50,000/= kwa siku
5.	Kabali kwa ajili ya sherehe	30,000/= kwa siku
6.	Ada ya waganga wa jadi waliosajiliwa	50,000/= kwa mwaka

**V. ADA NA USHURU WA STENDI NA MAEGESHO KWA MAENEKO  
YALIYOTENGWA**

<i>Na.</i>	<i>Chombo cha usafiri</i>	<i>Ushuru wa maegesho</i>
1.	Pikipiki iliyosajiliwa kwa Biashara katika maeneo yaliyotengwa	500/= kwa siku
2.	Teksi	1,000/= kwa siku
3.	Lori chini ya tani 7/ Pick up/ Basi dogo	1,500/= kwa siku
4.	Lori zaidi ya Tani 7/ Basi kubwa	2,000/= kwa siku
5.	Magari mengine yasiyo ya biashara	500/=kwa siku
6.	Ushuru wa kituo cha mabasi/stendi	
	i. Mabasi makubwa zaidi ya abiria 25	1,500/= kwa kutoka
	ii. Mabasi yanayobeba abiria chini ya 2	1,000/= kwa kutoka
	iii. Teksi/Gari dogo chini ya abiria 5	500/= kwa kutoka
	iv. Pikipiki/bodaboda/bajaji	300/= kwa kutoka
	v. Baiskeli	200/= kwa kutoka

**VI. ADA YA MATANGAZO YA BIASHARA**

	<i>Aina ya tangazo</i>	<i>Kiwango cha ushuru</i>
1.	Maombi ya kuweka mabango ya Biashara/kuchora	10,000/= kwa maombi
2.	Matangazo yanayong'aa	30,000/= kwa mwaka
3.	Matangazo yasiyong'aa	20,000/= kwa mwaka
4.	Ubao wa tangazo usiongaza kwa mita za mraba	20,000/= Kwa mwezi
5.	Bango la tangazo lisiloangaza kwa mita za mraba	50,000/= kwa

***Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi***  
***Tangazo la Serikali Na. 226 (linaendelea)***

		mwezi
6.	Bango la tangazo linaloangaza	90,000/= kwa mwezi
7.	Tangazo kwa kutumia kitambaa	60,000/= Kwa siku
8.	Matangazo ya ukutani kwa mita za mraba	30,000/= kwa siku
9.	Bango la tangazo linalobadilika badilika	200,000/= kwa mwaka
10.	Matangazo kwa njia ya maonesho(kutambulisha bidhaa,huduma	50,000/= kwa siku
11.	Matangazo ya vipaza Sauti/ Magari na Promosheni	30,000/= kwa siku
12.	Tangazo la Karatasi	1,000/= kwa siku

**VII. ADA NA USHURU WA SOKO NA MINADA**

A.	<i>Ada na Ushuru</i>	<i>Kwa siku</i>
1.	Ushuru wa sokoni kwa meza	300/=
2.	Ada na Ushuru wa minada	1,000/=
3.	Meza	1,000/=
4.	Wauza mitumba/nguo	1,000/=
5.	Mamalishe.	1,000/=
6.	Vinywaji	2,000/=
7.	Biashara ndogondogo.	500/=
8.	Vilabu nya pombe	1,000/=

  

B.	<i>Ada na kusafirisha mifugo</i>	<i>Kiwango cha ushuru</i>
1.	Ngombe (ndani ya Wilaya)	2,000/= kwa kila kichwa
2.	Ngombe (njie ya Wilaya)	15,000/= kwa kila kichwa
3.	Mbuzi (ndani ya Wilaya)	2,000/= kwa kila kichwa
4.	Mbuzi (njie ya Wilaya)	3,000/= kwa kila kichwa
5.	Kondoo (ndani ya Wilaya)	2,000/= kwa kila kichwa
6.	Kondoo (njie ya wilaya)	2,000/= kwa kila

***Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi***  
***Tangazo la Serikali Na. 226 (linaendelea)***

		kichwa
7.	Nguruwe (ndani ya Wilaya)	2,000/= kwa kila kichwa
8.	Nguruwe (nje ya Wilaya)	5,000/= kwa kila kichwa
9.	Kuku/bata/kanga (ndani ya Wilaya)	300/= kwa kila kuku,bata,kanga
10.	Kuku/bata/kanga (nje ya Wilaya)	500/= kwa kila kuku/bata/kanga
11.	Samaki (wakubwa)	2,000/= kwa ndoo ya lita 20
12.	Samaki (wadogo)	5,000/= kwa ndoo ya lita 20

C. Kodi ya nyumba za Halmashauri

1.	Nyumba daraja la kwanza	40,000/= kwa mwezi
2.	Nyumba daraja la pili	25,000/= kwa mwezi
3.	Nyumba daraja la tatu	10,000/= kwa mwezi

VIII. ADA YA VIBALI VYA UJENZI

1.	Ada ya huduma ya vibali vya ujenzi	10,000/= kwa kibali
2.	Ada ya maombi ya kumiliki kiwanja	10,000/= kwa kila fomu

IX. USHURU WA NGOZI

	<i>Aina ya mifugo</i>	<i>Kiwango cha Ushuru</i>
1.	Ng'ombe	200/= kwa kila ngozi
2.	Mbuzi	200/= kwa kila ngozi
3.	Kondoo	200/= kwa kila ngozi
4.	Wanyama wengine	200/= kwa kila ngozi

***Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi***  
***Tangazo la Serikali Na. 226 (linaendelea)***

**X. USHURU WA MAZAO YA MISITU**

	<i>Aina ya zao</i>	<i>Kiwango cha Ushuru</i>
1	Kuni za miti laini	7,500/= kwa tani
2	Mkaa	2,000/= kwa gunia
3	Mbao bila kujali unene na aina ya mti	300/= kwa ubao
4	Nguzo bila kujali unene na aina ya Mti	300/= kwa nguzo
5	Fito zinazosafirishwa nje ya Halmashauri	300/= kwa mzigo
6	Magogo ya Miti laini ya nguzo za umeme	1,000/= kwa gogo
7	Nguzo za umeme	1,500/= kwa nguzo 1
8	Asali	Asilimia 5 ya bei mauzo kwa kila lita moja
9	Magogo mete yanayotumika viwandani kwa ajili ya nishati ya moto	10,000/= kwa tani
10	Magogo yanayotumika kutoa nishati ya moto kiwandani	300/= kwa gogo

**XI. USHURU WA SHUGHULI ZA KIJASILIAMALI**

	<i>Aina ya shughuli</i>	<i>Kiwango cha Ushuru</i>
1	Mikokoteni	3,000/= kwa mwezi
2	Mafundi cherehani wakujitegemea	3,000/= kwa mwezi

***Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi***  
***Tangazo la Serikali Na. 226 (linaendelea)***

3	Wauza madawa ya jadi	3,000/= kwa mwezi
4	Mafundi viatu wa mitaani	3,000/= kwa mwezi
5	Wapiga picha wa mitaani	3,000/= kwa mwezi
6	Wauza maua, midoli na mapambo	3,000/= kwa mwezi
7	Mafundi baiskeli	3,000/= kwa mwezi
8	Wauza kanda za muziki kwenye matoroli	3,000/= kwa mwezi
9	Wamachinga wote	3,000/= kwa mwezi
10	Wachonga mihiuri	3,000/= kwa mwezi

**XII. USHURU WA MAZAO YA MITO, MAZIWA NA MABWAWA**

	<i>Aina ya Mazao</i>	<i>Kiwango cha Ushuru</i>
1	Samaki	Asilimia 5 ya bei ya zao
2	Mazao yote ya bahari, mito, maziwa na mabwawa	Asilimia 5 ya bei ya zao

**XIII. ADA NA USHURU WA HUDUMA YA UZOAJI TAKA**

1	Viwanda vikubwa	780,000/= kwa mwaka
2	Viwanda vidogo	260,000/= kwa mwaka
3	Hoteli	180,000/= kwa mwaka
4	Migahawa	60,000/= kwa mwaka

***Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi***  
***Tangazo la Serikali Na. 226 (linaendelea)***

---

5	Duka la jumla	60,000/= kwa mwaka
6	Nyumba za kuishi	12,000/= kwa mwaka
7	Masoko na Stendi	50,000/= kwa mwaka
8	Ada na ushuru wa dampo	5000/= kwa tripu
9	Ada ya huduma ya eneo la mazishi lililotengwa	2,000/=

**XIV. ADA YA USAJILI WA VYOMBO VYA USAFIRI VYA BIASHARA  
NDANI YA HALMASHAURI**

1	Daladala/Mzunguko	50,000/= kwa mwaka
2	Tax cab	40,000/= kwa mwaka
3	Gari binafsi ya kukodisha	45,000/= kwa mwaka
4	Gari aina nyingine	40,000/= kwa mwaka
5	Bajaji	30,000/= kwa mwaka

**HATI YA KUKIRI NA KUFILISHA KOSA**

---

*(Chini ya kifungu cha 8)*

---

Mimi ..... nakiri mbele ya .....ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Busokelo, kwamba mnamo tarehe ..... ya Mwezi ..... Mwaka ..... nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ..... cha Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo (Ada na Ushuru) za Mwaka 2014.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada/ Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi  
Tangazo la Serikali Na. 226 (linaendelea)

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA  
HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe..... ya Mwezi..... Mwaka .....

Jina..... *Saini*.....

Mbele ya :

Jina: .....

Cheo: .....

Saini: .....

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo uliofanyika tarehe 05/9/2013 mbele ya:-

.....  
IMELDA ISHUZA,  
*Mkurugenzi Mtendaji*  
*Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo*

.....  
MECKSON MOSES MWAKIPUNGA,  
*Mwenyekiti*  
*Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo*

NAKUBALI,

Dodoma,  
19 Mei, 2014

.....  
MHE. MIZENGO P. PINDA (Mb.)  
*Waziri Mkuu*